TOLEO LA 02

MACHI, 2024

# SUZA

CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR

www.suza.ac.tz

*Kichocheo cha Mabadiliko ya Jamii*




# JARIDA MAALUM LA MIAKA 60 YA MAPINDUZI

# Yaliyomo

1.0 Yaliyomo .................................................................................. 2

2.0 Dkt. Samia afurahishwa wanawake kuibuka vinara .......................... 3

3.0 Serikali yajivunia ongezeko la idadi ya wahitimu SUZA ..................... 4

4.0 Dk. Mwinyi awatunza waliobuni kuanzishwa SUZA ............................ 5

5.0 Matukio katika Picha ............................................................. 6

6.0 SUZA yaandaa Kongamano la Kitaaluma ........................................ 8

7.0 SUZA yashiriki maonesho kwa njia ya magari .................................. 9

8.0 SUZA yaacha alama Maonesho ya Nyamanzi 2024........................... 10

9.0 SUZA yashiriki kilele maadhimisho Mapinduzi ya Zanzibar ............. 11




# Dkt. Samia afurahishwa wanawake kuibuka vinara

***Na Mwandishi Wetu, SUZA***

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa wito kwa jamii kuunga mkono jitihada za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuongeza kasi ya ushawishi wa wanawake kujiunga katika fani mbalimbali za masomo.

Wito huo aliutoa katika sherehe za mahafali ya 19 ya SUZA katika ukumbi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, Tunguu - Mkoa wa Kusini Unguja, baada ya kutunukiwa Shahada ya Uzamivu ya Heshima ya Utalii na Masoko.

Dkt. Samia alisema hivi sasa wakati umebadilika na kwamba wanawake wamekuwa mstari wa mbele kujitafutia maendeleo yao na jamii kwa jumla. Katika mahafali hayo wahitimu 2,102 walitunukiwa vyeti katika ngazi mbalimbali ambapo miongoni mwao 1,229 ni wanawake sawa na asilimia 61 ya wahitimu.

'Mafanikio haya yametokana na juhudi zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuleta usawa wa kijinsia. Wakati wetu wanawake kila tukienda juu (elimu ya juu) tunapungua leo imekuwa tafauti', alisema kwa fahari.

Akizungumzia mchango wake katika maendeleo ya Zanzibar, Dkt. Samia alisema tunzo aliyopokea ni heshima kwa Watanzania wote katika kutekeleza majukumu yao. Aliongeza kuwa katika kufanya kazi zake, alishirikiana na watu mbalimbali na kubadilishana nao mawazo na kubaini kuwa walifanya mambo mengi makubwa ya kuing'arisha nchi.

'Wakati tunafanya yote haya, hatukuwaza kama juhudi zile zitajulikana na kutunukiwa heshima kubwa namna hii', alisema. Alisema kuwa miongoni mwa viongozi waliompaisha ni Rais Mstaafu wa Awamu ya Sita Dkt. Amani Abeid Karume, ambaye ndiye alimteua kushika nafasi ya Uwaziri katika masuala ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto na baadae Waziri wa Utalii Biashara na Uwekezaji.

"Nilitolewa kichochoroni nikapewa Wizara inayoshughulikia masuala ya Wanawake na Watoto na baadae Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji. Heshima hii ni kwa bosi wangu, Dkt. Amani Karume, nashukuru kwa malezi uliyonipa na leo napata heshima kubwa", alimshukuru huku akimuangalia Dkt. Karume.

Akitoa nasaha zake kwa wahitimu, Dkt. Samia aliwataka kwenda kwenye jamii na kuzikabili changamoto zilizoko kwenye jamii.

Awali Dkt. Ali Makame Ussi, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi alisoma wasifu wa Dkt. Samia Suluhu Hassan uliosheheni juhudi na mchango wake kwa maendeleo ya Taifa ikiwemo msukumo mkubwa alioutoa katika kukuza sekta ya utalii.

Kwa upande wake, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alieleza kuridhishwa kwake na kuwepo idadi kubwa ya wahitimu wanawake wanaofanya vizuri katika masomo yao. "Nachukua fursa hii kukupongezeni tena wahitimu wetu hasa wanawake ambao kwa mara nyengine mmetokea kuwa ndiyo wengi kuliko wanaume, wahitimu wanawake ndio wanaoshika nafasi nyingi za juu katika masomo mbali mbali", alisema Dk. Mwinyi.

Mapema Makamu Mkuu wa SUZA, Prof. Moh'd Makame Haji alisema Chuo kimeandaa programu mpya ya Ujasiriamali na Ubunifu ambapo kati ya wahitimu 18 waliotunukiwa vyeti wahitimu 16 ni wanawake.

Katika hatua nyengine, Chuo kimetoa wanafunzi bora ambao wote ni wanawake kwa kila ngazi: Shahada ya Kwanza (Rose R. Kibiriti wa fani ya Afya ya Mazingira), Stashahada (Farhia Farhan Juma wa fani ya Kinywa na Meno) na ngazi ya Astashahada (Khadija Paquet wa fani ya TEHAMA).



# Serikali yajivunia ongezeko la idadi ya wahitimu SUZA

***Na Mwandishi Wetu, SUZA***

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesifu jitihada za SUZA zinazochangia kuongezeka idadi ya wahitimu mwaka hadi mwaka.

Akitoa hotuba yake mbele ya wahitimu, viongozi na wageni kwenye mahafali ya 19 katika ukumbi wa Dkt. Ali Mohamed Shein huko Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja Dk. Mwinyi ambaye ndiye Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), alisema anaamini kuwa wahitimu hao wameandaliwa vyema ili kuingia kwenye ushindani wa soko la ajira.

Akifafanua kuhusu ongezeko hilo, Dk. Mwinyi alisema katika mahafali hayo jumla ya wahitimu 2,102 wametunukiwa vyeti katika ngazi mbalimbali ikiwa ni ongezeko la asilimia tisa ikilinganishwa na idadi ya wahitimu 1,913 wa mwaka uliopita. Aidha, alipongeza jitihada za wanawake kuichangamkia sekta ya elimu ya juu ambapo kati ya waliohitimu wanawake ni 1,229 sawa na asilimia 61.

"Napenda niupongeze uongozi wa Chuo, wahadhiri, wafanyakazi na uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mafanikio ambayo Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinaendelea kuyapata katika kusukuma mbele maendeleo ya nchi yetu", alisema.

Aidha, Dk. Mwinyi alielezea kuridhishwa kwake na kuwepo programu mpya ya Ujasiriamali na Ubunifu (*Bachelor of Entrepreneurship and Innovation*) ambapo wahitimu 18 aliwatunuku Shahada zao wakiwemo wanawake 16 sawa na asilimia 89.

Katika mahafali hayo, wahitimu waliotunukiwa vyeti walikuwa ni wa ngazi za Shahada ya Uzamivu, Shahada za Uzamili, Shahada za kwanza, Stashahada na Astashahada.

Katika mahafali hayo, Dk. Mwinyi pia alimtunuku Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Shahada ya Uzamivu ya Heshima ya Usimamizi wa Utalii na Masoko (*Doctor of Philosophy in Tourism Management and Marketing -Honoris Causa*) kutokana na mchango mkubwa alioutoa katika sekta ya utalii inayoendelea kusukuma maendeleo ya taifa kwa kasi.

Katika hatua nyengine, Dk. Mwinyi aliwatunuku tunzo maalum za heshima viongozi wengine waliopanda mbegu za uanzishwaji wa SUZA ikiwa ni sehemu ya kuthamini mchango wao. Viongozi hao ni Rais Mstaafu wa Awamu ya Tano wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dkt. Salmin Amour Juma ambaye ndiye kinara aliyetoa wazo hilo.

Wengine ni Mawaziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali katika vipindi tafauti ambao ni Mhe. Haroun Ali Suleiman na Balozi Omar Ramadhan Mapuri. Aidha, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kwa muda mrefu Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee naye pia ana mchango mkubwa wa uratibu hadi wazo hilo kutekelezeka.

Mapema, akimkaribisha Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Lela Muhammed Mussa alielezea mafanikio yaliyopatikana katika Chuo hicho kama vile kuwapatia mafunzo wahadhiri katika ngazi mbalimbali za mafunzo na Serikali kuwalipia ada za masomo wafanyakazi zaidi ya 100 wa SUZA.

Aliongeza kuwa wahadhiri hao wapo masomoni kwenye ngazi mbalimbali kama vile Shahada ya Uzamivu 47, Shahada ya Uzamili 37, Shahada ya kwanza 15 na Astashahada mfanyakazi mmoja.

Alifafanua kuwa, kupitia SUZA Serikali imeanzisha maabara ya ubunifu (*WASTEX Lab*) Tunguu pamoja na kununua vifaa vya maabara vikiwemo Kompyuta na TEHAMA.

Mapema, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Moh'd Makame Haji aliipongeza jumuiya ya Chuo ikijumuisha wanataaluma na waendeshaji kwa kazi nzuri wanayofanya ya kutoa wataalamu wa fani mbalimbali wanaotarajiwa kuwa mhimili mkubwa katika kuchangia ustawi wa nchi.




# Dk. Mwinyi awatunza waliobuni kuanzishwa SUZA

***Na Mwandishi Wetu, SUZA***

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi amewatunuku tunzo maalum viongozi na wataalamu waliobuni fikra ya kuanzishwa na kuimarishwa kwa SUZA.

Tunzo hizo zilitolewa kwa niaba yake na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, Mhe. Jamal Kassim katika uzinduzi wa Mkusanyiko wa Kwanza wa Kitaaluma (*Convocation*) wa Chuo hicho uliofanyika katika Kampasi ya SUZA Maruhubi ikiwa ni miongoni mwa shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Mwinyi ambaye pia ni Mkuu wa SUZA alikipongeza Chuo kwa kukamilisha azma ya kuunda Mkusanyiko wa Kitaaluma. Aliongeza kuwa Mikusanyiko ya Kitaaluma ya vyuo vilivyofanikiwa duniani vimeweza hata kuwa na vyanzo vya mapato imara vinavyoweza kusimamia na kushauri katika shughuli za maendeleo na kitaaluma za vyuo vinavyohusika.

"Kuanzisha Mkusanyiko wa Kitaaluma ni jambo linalohitaji kujikubalisha kwa walengwa kutokana na ukweli kwamba Mkusanyiko wa Kitaaluma unasimama kama taasisi yenye Kamati za Utendaji na usimamizi wa mipango yake ambayo inahitaji muda wa kutosha ili kufanikisha majukumu yake", alisisitiza Mkuu wa Chuo.

Aidha, Dk. Mwinyi alifahamisha kuwa hivi sasa dunia inapiga hatua za maendeleo kwa kutumia wasomi zaidi katika kufanikisha utayarishaji na utekelezaji wa sera na mipango ya kimaendeleo ya nchi mbalimbali, hivyo, ana matumaini kuwa wanataaluma na wote waliohitimu, wataitumia vizuri fursa hii ya Mikusanyiko ya kitaaluma kuleta mabadiliko chanya kwa jamii ya SUZA na Zanzibar kwa ujumla.

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kilianzishwa miaka 22 iliyopita ambapo chimbuko la kuundwa kwake lilitokana na fikra za Mhe. Alhaj Dkt. Salmin Amour Juma, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tano ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Dkt. Mohammed Gharib Bilal, Waziri Kiongozi Mstaafu ambao SUZA inautambua mchango wao ulioifikisha Zanzibar kuwa kitovu cha kuzalisha wasomi na wataalamu kwenye fani mbalimbali.

Katika hatua nyengine, Mhe. Dkt. Amani Abeid Karume Rais Mstaafu wa Awamu ya Sita wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ameonesha jitihada za kukiimarisha Chuo hiki sambamba na Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi ambaye ni Mkuu wa Chuo wa kwanza kuanzisha Mkusanyiko wa Kitaaluma.

Halikadhalika, mawaziri vinara wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar katika vipindi tafauti waliosimamia kuikuza fikra ya Dkt. Salmin Amour ni Mhe. Haroun Ali Suleiman, Mhe. Omar Ramadhan Mapuri, Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee wakati huo akiwa Katibu Mkuu katika Wizara hiyo kwa kipindi kirefu alisimamia Kamati za Uratibu wa Uanzishwaji wa SUZA.

Vilevile, SUZA inatambua michango ya wanakamati akiwemo Prof. Saleh Idris Muhammed Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya SUZA na Dkt. Said Gharib Bilal akiwa Katibu wa Kamati hiyo. Wajumbe wengine wa Kamati hiyo ni Dkt. Bishara Theneyan Mohammed, Dkt. Ibrahim Said Rashid Msabaha, Marehemu Bw. Ahmed Mohammed Abdulrahman, Prof. Abdul Sheriff, Prof. Ali Seif Mshimba, Marehemu Prof. Haroub Miraji Othman na Prof. Geoffrey Rafael Vehaeli Mmari.

Aidha, tunzo nyengine maalum ilitolewa kwa Bw. Said Salim Bakhresa kwa kutambua mchango wake kwa jamii ya SUZA katika harakati za awali za uimarishaji wa Chuo hicho.

Katika upangaji safu wa kukiendeleza Chuo hicho, mchango wa wajumbe wa sekretarieti ya uanzishwaji wa SUZA pia inathaminiwa ambao ni Bi. Maimuna Rashid Shaaban, Bw. Waadili P. L. Kavishe, Bi. Rabiya Tajiri Ali ambao pia walitunukiwa tunzo za heshima.

Mapema, Makamu Mkuu wa SUZA, Prof. Moh'd Makame Haji, alisema kuwa Mkusanyiko wa Kitaaluma unalenga kuchochea mabadiliko na maendeleo kwa ujumla. Miongoni mwa malengo hayo ni kuimarisha na kukuza ushirikiano baina ya wadau mbalimbali wa SUZA, kuimarisha ustawi, hadhi, ubora na maendeleo ya Chuo, kujadili na kushauri mambo mbalimbali kwa ustawi wa SUZA.

Uongozi wa SUZA na wafanyakazi wote unawapongeza waliobuni fikra ya kuanzishwa Chuo kwa mbegu bora walizozipanda zinazoendelea kutoa mavuno mazuri ya kujivunia.

# *Matukio katika Picha*




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, Mhe. Jamal Kassim akiwa katika Picha ya pamoja na Wanajumuiya wa SUZA katika Mkusanyiko wa Kwanza wa Kitaaluma (*Convocation*) uliofanyikakatika Kampasi ya SUZA Maruhubi




Mwananchi akipatiwa Huduma ya Upimaji *(Presure)* ndani ya banda la SUZA katika Maonesho ya Biashara na Tamasha la 10 la Biashara Zanzibar, Nyamanzi Wilaya ya Magharibi "B" Mkoa wa Mjini Magharibi.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda akizungumza katika Kongamano la Kitaluma lililoandaliwa na SUZA.




Trekta la SUZA pamoja na gari yakiandaliwa kwa ajili ya maonesho ya bidhaa na huduma ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za Miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.




# SUZA yaandaa Kongamano la Kitaaluma

***Na Mwandishi Wetu, SUZA***

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda alisema Vyuo Vikuu vina jukumu la kuichambua historia kwa uwazi na kiuzalendo ili kuepuka upotoshaji.

Hayo aliyasema wakati akifungua Kongamano la Kitaaluma lililoandaliwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) katika Ukumbi wa Dkt. Ali Mohamed Shein Tunguu - Mkoa wa Kusini Unguja ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za maadhimisho ya miaka sitini (60) ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Prof. Mkenda alisema historia ni uwanja wa mapambano na inatoa fursa kwa watu kuchora picha mbalimbali. Aliongeza kuwa Mapinduzi katika nchi yoyote duniani hufanyika kwa lengo la kubadilisha mfumo na kama zilivyo nchi nyengine, Zanzibar imeitumia dhana hiyo kuleta usawa wa binadamu. “Tuna jukumu la kuiangalia kwa macho meupe, uhakika na ukweli tusije kusababisha vizazi vijavyo kuwa na tafsiri tafauti”, alisisitiza.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Mhe. Haroun Ali Suleiman, alihimiza kufundishwa historia ya Zanzibar kwa wananchi mbalimbali hasa kupitia kwenye taasisi za elimu. “Muelewe historia ya nchi yenu kwani skuli haisomeshwi kama inavyostahiki. Someni huu ndio wakati wenu”, alikumbusha. Akizungumzia maendeleo ya elimu Zanzibar, Mhe. Haroun alisema Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kilianzishwa miaka 22 iliyopita kikiwa na wanafunzi 54 na sasa kina wanafunzi zaidi ya 7,000. Mhe. Haroun aliongeza kuwa kabla ya Mapinduzi kama hujulikani huwezi kupata elimu na mwenye asili fulani anayeishi mjini ni tafauti na anayeishi shamba, hali ambayo kwa sasa ni tafauti. Aidha, alishauri kuwa makongamano kama hayo yafanyike kwenye Wilaya za Unguja na Pemba ili wananchi wengi zaidi nao wapate taaluma ya historia ya nchi yao.

Akichangia mada kuhusu harakati za ukombozi Zanzibar na Afrika, Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Mhe. Stephen Wasira, alisema Mzee Karume alichukia dhulma na alipenda haki.

Aliongeza kuwa, Mzee Karume aliamini katika umoja na hivyo kuungana na viongozi wengine wa Afrika ili kupigania uhuru kwa pamoja. “Mapinduzi haikuwa ajali ilikuwa lazima yafanyike kwa njia ya amani yasingekuwa. Historia huwezi kuibadilisha, ukiibadilisha utaandika unavyotaka lakini historia itabaki palepale”, Mhe. Wasira alikumbusha.

Akimkaribisha mgeni rasmi, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA), Bw. Khamis Abdulla, alisema miongoni mwa kazi za Chuo Kikuu ni kuchechemua fikra ambapo leo wasomi na wabobezi wana fursa ya kujadili historia, maendeleo na mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka 60 iliyopita.

Akichangia mada ya wasifu wa Hayati Mzee Abeid Amani Karume, Bw. Ali Shaaban Juma ambaye ni msomi na mtunzi wa vitabu alisema, Mzee Karume alijenga misingi imara ya kuwaweka watu pamoja kwa kuondoa dhana ya kujiona bora hali ambayo inasababisha kuleta mfarakano. Alifafanua kuwa nchi kadhaa zilikuwa na tawala za jadi, kikabila au kidini zilizojiona kuwa ni bora hivyo kupambana na makundi mengine. “Baada ya Mapinduzi Mzee Karume alifuta dhana ya kujiona kuwa mimi ni bora kwani ikifikia hapo huishia kuuana”, alisistiza

Naye Bi. Ziada Mussa ambaye ni Mkufunzi wa somo la historia kampasi ya Tunguu, alisema kuwa amejifunza mambo mengi ambayo hakuwahi kuyasikia katika historia ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, alipendekeza makongamano kama haya kuwa endelevu ili kuepusha kuharibiwa historia lakini pia kuwajenga vijana kizalendo.

Kwa upande wake Bw. Samuel Nathania ambaye ni mwanafunzi wa mwaka wa kwanza kutoka Kampasi ya Nkrumah, alisema hakuwahi kuifahamu historia ya Mapinduzi ya Zanzibar kwani yeye siyo mzaliwa wa Zanzibar, ila amevutiwa na mada zote zilizowasilishwa. Aliongeza kuwa ameona faraja pia kongamano kuwashirikisha viongozi waliobobea katika masuala mbalimbali ya kitaaluma.

Kongamano hilo lililobeba kauli mbiu ‘Tuimarishe Uchumi, Uzalendo na Amani kwa Maendeleo ya Taifa Letu’, liliongozwa na Balozi Mohammed Hamza, lilipambwa na utenzi wa papo kwa papo ulioghaniwa na Bw. Kassim Yussuf (Zirokasorobo), lilihudhuriwa na wageni mbalimbali akiwemo, Naibu Katibu Mkuu Mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi, Dk. Abdalla Juma Sadalla (Mabodi), na wanajumuiya wa SUZA. Wengine ni; wanafunzi na wanataaluma kutoka Chuo Kikuu cha Alsumait, Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU), Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Karume (MNMA), Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (KIST), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na Chuo cha Kiislamu Zanzibar (CCK).

Washiriki wengine ni wawakilishi wa Jumuia za vyama vya siasa Tanzania, ACT - Wazalendo, ADA TADEA, CHADEMA, wazazi, vijana, wanawake na waandishi wa habari.




## SUZA yashiriki maonesho kwa njia ya magari

***Na Mwandishi Wetu, SUZA***

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kimeungana na taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi kushiriki katika aonesho ya bidhaa na huduma kwa kutumia magari (*Road show*).

Maonesho hayo yakiwa ni miongoni mwa shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, yalijenga hamasa kwa wananchi kujitokeza kwa wingi katika maeneo yote ambayo msafara wa magari hayo ulipita.

Katika maonesho hayo huduma na kazi zinazofanywa na taasisi zilioneshwa. Wananchi nao walionesha kuvutiwa nayo kutokana na jinsi walivyokuwa wakishangiria na kupunga mikono yao huku baadhi wakipata kumbukumbu kwa kupiga picha kwa kutumia simu zao.

Kwa upande wa SUZA kupitia magari yake, wananchi walikagua bidhaa na huduma mbalimbali likiwemo Trekta la Skuli ya Kilimo iliyoko Kizimbani, ambapo walishangazwa na mkungu mkubwa wa ndizi uliotokana na mgomba maarufu aina ya Ali Hassan Mwinyi uliokuwa na madole makubwa 22.

Kwa mujibu wa mtaalamu wa Kilimo kutoka Skuli hiyo, Bw. Mzee Kombo, aliwaeleza wananchi kuwa mara nyingi aina hiyo ya ndizi hutoa dole moja ama matatu hali inayotokana na ukosefu wa huduma bora za mgomba kama vile maji na shimo la mgomba kuwa dogo.

Hata hivyo, kutokana na Chuo kuwa na jukumu la kutoa elimu ya kilimo kimeonesha kuwa inawezekana kwa aina hiyo ya mgomba kutoa madole mengi zaidi ya ilivyozoeleka. Aidha, gari nyengine ya Chuo iliyowavutia watu wengi ni ya Skuli ya Afya na Sayansi za Tiba ambapo kulikuwa na sanamu la mgonjwa aliyelazwa kitandani akionekana kuwa hali mbaya na huku akiongezewa damu.

Halikadhalika, Taasisi ya Utalii ya SUZA ilionesha aina za vyakula ambavyo vilivutia watu wengi hasa watoto waliokuwa wakitamani kuvionja huko wakisikika kusema "kateni keki tule".

Pia, Skuli nyengine za Chuo zilizoonesha shughuli zao ni Skuli ya Elimu na Idara ya Habari na Mawasiliano iliyo chini ya Skuli ya Kompyuta, Mawasiliano na Mafunzo ya Habari.

Maonesho hayo yalishirikisha zaidi ya gari 60 kutoka taasisi mbalimbali za serikali na sekta binafsi. Watu wengi walifurahishwa na maonesho hayo kwa kuwa wengi wao hawakuwa wakifahamu huduma na bidhaa zinazotolewa na taasisi hizo, hivyo maonesho hayo yalitoa elimu tosha kwa wananchi.

Wananchi walijipanga barabarani zilimopita gari hizo kuanzia viwanja vya Amani kupitia kwa Juma Pweza, Saateni, Gulioni, Malindi, Darajani, hadi viwanja vya Mnara wa Kumbukumbu ya Mapinduzi Kisonge ambako yalipokewa na Makamu wa Pili wa Rais Mstaafu Balozi Seif Ali Iddi na kumalizikia viwanja vya Maisara ambako gari zote za maonesho baadae zilitawanyika.

Akizungumza na wanahabari Balozi Seif alipongeza jinsi maonesho hayo yalivyofana na kupendekeza kuwa ni vyema yakawa endelevu. Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Mhe. Mudrik Ramadhan Soraga, alisema kuwa kutokana na mwamko uliooneshwa na taasisi zilizoshiriki Serikali inatarajia maonesho mengine kufanyika kwenye maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani mwaka huu.




# *SUZA yaacha alama Maonesho ya Nyamanzi 2024*

***Na Mwandishi Wetu, SUZA***

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ni miongoni mwa taasisi zilizoshiriki Maonesho ya Biashara na Tamasha la 10 la Biashara Zanzibar, Nyamanzi Wilaya ya Magharibi "B" Mkoa wa Mjini Magharibi, ikiwa ni katika shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Maonesho hayo yaliyofanyika kwa muda wa wiki mbili kuanzia tarehe 7 hadi 19 Januari mwaka huu, yalifunguliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi, na kubeba ujumbe 'Tuimarishe Uchumi, Uzalendo na Amani kwa Maendeleo ya Taifa.

SUZA iliacha alama kwa wananchi wengi kuvutiwa na huduma zinazotolewa na Skuli zake zilizoshiriki maonesho hayo. Kwa upande wa washiriki wa kutoka Taasisi ya Utalii Maruhubi, wafanyakazi wanaotoa huduma za hoteli walionesha aina mbalimbali za kupamba kitanda.

Wafanyakazi hao walionesha 'design' hizo na kuwafundisha watu waliohudhuria kwenye maonesho hayo huku wakiwashawishi kujiunga na Chuo chao ili wajifunze mambo mapya na ya kisasa ya utunzaji wa nyumba.

Huduma nyengine zilizotolewa na Taasisi ya Utalii ni vyakula vya aina mbalimbali na vinywaji ambavyo viliuzwa kwa wananchi waliohudhuria maonesho. Maofisa katika Skuli ya Kilimo, walionesha jinsi ya kutunza mashamba sambamba na kuuza miti mbalimbali ya matunda na bustani. Vilevile walionesha baadhi ya bidhaa wanazozalisha zilizo katika ubora wa hali ya juu.

Aidha, Skuli ya Kompyuta, Mawasiliano na Mafunzo ya Habari walitengeneza mfano wa chumba cha kutoa huduma za chumba cha uangalizi maalum (Neonatal) na namna ambavyo kinaweza kutoa ishara ya dharura inapotokea ili muuguzi afike haraka kutoa huduma inayostahiki.

Kwa upande wa Skuli ya Kiswahili, walionesha machapisho mbalimbali pamoja na mafunzo ya lugha yanayotolewa kwa wageni na wenyeji wanaotaka kujifunza Kiswahili, Kiingereza, Kichina, Kihispania, Kireno, Kiarabu, Kikorea na Kifaransa ambapo Skuli hiyo imeongeza umaarufu wake kwa kupokea wageni kutoka nchi mbalimbali wanaokuja kujifunza lugha na kufanya utafiti wa lugha ya Kiswahili. Skuli ya Biashara nao, walijitokeza kuwaonesha wageni aina mbalimbali za bidhaa walizokuwa wakizalisha kama vile bidhaa za urembo na chakula.

Miongoni mwa bidhaa hizo ni unga wa muhogo, unga wa ulezi, unga wa mtama, viungo vya kupikia, mafuta ya mgando, manukato, na aina nyengine za mapambo.

Aidha, pamoja na kuonesha bidhaa hizo SUZA ilikabiliwa na changamoto ya ukosefu wa eneo la kutosha kuonesha huduma zake kutokana na kupangiwa mahali padogo.

Kwa hivyo, skuli hizi zilikuwa zikipangiana siku za kushiriki maonesho na hivyo kuonesha huduma zake kwa kupishana. Hali hii iliwavunja moyo baadhi ya wananchi ambao walifika siku iliyofuata na kubaini kuwa huduma walizozifuata siku hiyo hazikuwepo kwani SUZA ililenga kuzishirikisha skuli zote.




# SUZA yashiriki kilele maadhimisho Mapinduzi ya Zanzibar

***Na Mwandishi Wetu, SUZA***

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kimeshiriki kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yaliyofanyika katika viwanja vya Amani mjini Zanzibar tarehe 12 Januari mwaka huu.

Viongozi wa Serikali akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mabalozi wa nchi mbalimbali waliopo Zanzibar, viongozi wa vyama vya siasa na mashirika ya serikali na umma walialikwa na kushiriki katika maadhimisho hayo.




Aidha, wanafunzi na wafanyakazi wa SUZA walishiriki kikamilifu kwenye maandamano wakiungana na wafanyakazi wa Serikali na taasisi binafsi waliopita mbele ya mgeni rasmi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi pamoja na viongozi wengine wa serikali.

Wanajumuiya kutoka SUZA walijitokeza na mabango yaliowatambulisha na kubeba ujumbe wa Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi unaosisitiza kuimarisha uchumi, uzalendo na amani kwa maendeleo ya taifa letu.




Wafanyakazi na Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) wakiwa katika maandamano kwenye Sherehe za Miaka 60 ya Mapinduzi.

# KAMATI YA JARIDA

## Mwenyekiti
Ndg. Hassan Simba Hassan

## Mratibu
Ndg. Khadija Sadiq Mahumba

## Mhariri wa Makala
Dkt. Masoud Nassor Mohammed

## Mhariri wa Habari
Dkt. Rashid Maalim Khamis

## Mtayarishaji wa Habari
Ndg. Nasima Haji Chum

## Mpiga Picha
Ndg. Hamza Makame Ussi

## Msanifu Jarida
Ndg. Zedi Abdalla Khamis

**Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar - SUZA**

www.suza.ac.tz

vc@suza.ac.tz